JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

**MAMLAKA YA UDHIBITI WA MAWASILIANO TANZANIA**

ISO 9001:2015 CERTIFIED

**KATIKA KAMATI YA MAUDHUI YA MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA, DAR ES SALAAM**

**SHAURI NA. 01 - 2023/2024**

**DHIDI YA**

**WASAFI FM COMPANY LIMITED (WASAFI FM RADIO)**

**UAMUZI WA KAMATI YA MAUDHUI JUU YA TUHUMA ZA UKIUKAJI WA KANUNI ZA MAWASILIANO YA KIELEKTRONIKI NA POSTA (MAUDHUI YA UTANGAZAJI WA REDIO NA TELEVISHENI), 2018 KAMA ILIVYOFANYIWA MAREKEBISHO MWAKA 2020.**

---

## 1.0 UTANGULIZI:

1.1 Tarehe 02 Machi, 2021, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ilitoa leseni kwa Kituo cha Utangazaji cha **Wasafi FM Company Limited (Wasafi FM Radio)** kwa ajili ya kutoa huduma ya utangazaji wa maudhui kwa njia ya redio nchini Tanzania.

1.2 Kwa mujibu wa Kanuni ya 45 (2) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, 2018 kama ilivyofanyiwa Marekebisho Mwaka 2020, Kamati ya Maudhui ya Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania ina jukumu la kusimamia watoa huduma wote wa maudhui ya utangazaji ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua stahiki za kisheria dhidi ya mtoa huduma yeyote atakayekiuka Kanuni za Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni au Sheria nyingine.

1.3 Mnamo tarehe 02 Novemba, 2023, **Wasafi FM Radio** kupitia kipindi cha **"Jana na Leo"** kinachotangazwa na watangazaji, **Oscar Oscar, Adella Tillya na Revocatus Chipando** anayejulikana kama **Baba Levo** walijadili kuhusu mvua zilizokuwa zikinyesha jijini Dar es salaam na katika mjadala huo walidai kuwa mvua hizo zilikuwa zikiamsha akili na kusababisha kuhitaji '***Mzagamuano***'.

1.4 Katika kipindi tajwa, mtangazaji **Revocatus Chipando** alisikika akitumia lugha isiyo sanifu, au inayoweza kutafsiriwa kama matusi au yenye kuhamasisha ufanyaji wa ngono, hususani kipindi cha mvua, jambo ambalo linaweza kuwafanya vijana na watoto kujaribu au kuiga tabia zisizofaa.

1.5 Mtangazaji **Revocatus Chipando** alisikika akisema maneno yafuatayo: -

"***Revocatus Chipando***: *... mvua inaendana sana na neno 'mzagamuo' yaani mvua na mzagamuo ni the same, yaani inaondoka kwa pamoja. We sema tu mvua ikinyesha, inaleta baridi, inatengeneza msisimko kwenye akili baada ya hapo akili ikishapata msisimko kuna kitu kinaingia katikati kinaitwa mzagamuo. Mzagamuo huwa inatengenezwa kwa aina mbili, unaweza kuamua kujizagamua mwenyewe ukiwa katika mambo yako ya kutumia simu ya mkononi au ukatafuta mwenza....*"

***Oscar:*** *lakini moja kati ya Kanuni ambayo nadhani imepitwa na wakati ni kanuni ya mahotel, guest na lodge kumpa mtu chumba kwa masaa 24. Saa 4 asubuhi ndio hotel na lodge nyingi wageni wanaingia kutoka ni kesho yake saa 4 asubuhi. Ingekuwa siku za mvua kama hizi mtu ukipate chumba hata kwa masaa manne uende ukapumzike mvua ikikatika unarudi nyumbani kwako. Upungufu umekuwa ukienda kwenye kila lodge kwenye kila guest pamejaa...*"

1.6 Kitendo cha kutangaza kipindi chenye maudhui yaliyotumia lugha isiyo sanifu au rasmi na isiyo na staha na inayoweza kutafsiriwa kama yenye kuhamasisha ufanyaji wa vitendo vya ngono wakati wa mvua, Kituo cha **Wasafi FM Radio** kinatuhumiwa kukiuka Kanuni ya 5(d) 11(1) (c), 12(1) (a), (d), na 29 (d) na (e) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni 2018, ambazo zinasomeka kama ifuatavyo:

*5.(d)- A commercial free-to-air content services provider shall promote the use of standard Kiswahili and English languages;*

*11.-(1) A licensee shall ensure that the programme and its presentation-*

*(c) observes good taste and decency;*

*12.-(1) A content services licensees shall-*

*(a) ensure that due care is exercised in order to avoid content which may disturb or be harmful to children;*

*(d) protect children from negative influences.*

*29. A content services licensee shall-*

*(d) avoid use of indecent and abusive language in programme presentation;*

*(e) avoid using improper language, pronunciations, or mixing of languages.*

## 2.0 WITO WA KUTOA MAELEZO YA UTETEZI

2.1 Tarehe 21 Novemba, 2023, Kamati ya Maudhui iliuandikia uongozi wa **Wasafi FM Radio** wito wa kuwasilisha mbele ya Kamati maelezo au utetezi wa kimaandishi pamoja na kufika mbele ya Kamati tarehe 28 Novemba, 2023 Saa 04:00 Asubuhi, ili kujieleza ni kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria kwa tuhuma hizo zinazowakabili.

2.2 Tarehe 28 Novemba, 2023, Saa 04:00 Asubuhi, **Wasafi FM Radio** ikiwakilishwa na **Bw. Nelson Kisanga**, Mkurugenzi wa Vipindi; ambaye aliambatana na **Orest Kawau**, Mkuu wa Maudhui; **Edo Kumwembe** na **Adella Tillya** ambao ni watangazaji wa kipindi cha *Jana na Leo*, walifika mbele ya Kamati ya Maudhui kwa ajili ya kutoa utetezi wao kwa nini wasichukuliwe hatua za kisheria.

## 3.0 UTETEZI WA WASAFI FM RADIO

3.1 Katika utetezi wao wa maandishi na kwa njia ya mdomo, Uongozi wa **Wasafi FM Radio** ulikiri kosa na pia kuomba radhi. Aidha, Bw. Orest Kawau alidai kuwa Uongozi wa Kituo hicho ulichukua hatua za haraka za kuzuia

mjadala huo usiendelee na kuziondoa nakala (clips) za kipande hicho cha maudhui kutoka kwenye mitandao yao ya kijamii kwa lengo la kuzuia kusambaa zaidi kwa maudhui hayo.

3.2 Vile vile, Bw. Kawau alidai kuwa Uongozi wa Kituo hicho umechukua hatua za kuhakikisha kuwa kosa kama hili halijirudii tena ambapo Uongozi wa **Wasafi FM Radio** uliandika barua za onyo kali kwa Bw. Oscar Oscar kwa kosa la kuanzisha mjadala usio na afya, wala tija kwa jamii na hivyo kumtaka kuhakikisha anafuata mwongozo wa kipindi.

3.3 Halikadhalika, katika utetezi wao, Uongozi wa Kituo cha **Wasafi FM Radio** walidai kuwa Mtangazaji (mhamasishaji), **Bw. Revocatus Chipando** anayejulikana kama **Baba Levo** alikutwa na hatia kwa kutumia lugha isiyo na staha na hivyo kusimamishwa kazi kwa muda wa wiki mbili kuanzia tarehe 20 Novemba, 2023 hadi tarehe 04 Desemba, 2023. Hii ni sambamba na kumuweka chini ya uangalizi ambapo hatua kali zaidi zitachukuliwa dhidi yake endapo atafanya kosa jingine. Pia, Uongozi wa **Wasafi FM Radio** uliambatisha barua walizoandikiwa Oscar Oscar na Baba Levo katika utetezi wao wa maandishi.

## 4.0 TATHMINI YA KAMATI

4.1 Kamati ya Maudhui imebaini kwamba **Wasafi FM Radio** imefanya kosa la kurusha maudhui yenye kutumia lugha isiyo sanifu, au inayoweza kutafsiriwa kama matusi au yenye kuhamasisha ufanyaji wa ngono, hususan kipindi cha mvua na isiyokuwa na staha mbele ya jamii kutokana na uzembe wa wasimamizi na watangazaji wa kituo hicho kwani walitakiwa kuwa makini na kuzingatia Sheria, Kanuni na Maadili ya Utangazaji.

4.2 Aidha, Kamati imebaini kuwa endapo **Wasafi FM Radio** wangezingatia Sheria, Kanuni, Weledi na Maadili ya Utangazaji wa Habari, ikiwa ni pamoja na kuwa na mwongozo wa kipindi (script), wangeweza kuepuka kurusha maudhui yasiyofaa, yenye kutumia lugha isiyo sanifu na inayoweza kutafsiriwa kama matusi au yenye kuhamasisha ufanyaji wa ngono

hususan kipindi cha mvua. Kuwepo kwa mwongozo wa kipindi kungesaidia na kuhakikisha watangazaji wanazingatia mwongozo wa kipindi husika, na hivyo kuepusha watangazaji kuanzisha mijadala yao wenyewe ambayo iko nje ya mwongozo (script) wa kipindi husika.

4.3 Kamati imebaini kuwa Kituo cha **Wasafi FM Radio** kina tatizo la usimamizi na uhariri wa vipindi vyao; jambo lililosababisha kurusha maudhui yenye ukakasi, yasiyotumia lugha fasaha na yenye ukiukwaji mkubwa wa Maadili na Kanuni za Utangazaji.

4.4 Pia, Kamati imebaini kuwa Kituo cha **Wasafi FM Radio** kina tatizo la kuwa na baadhi ya watendaji/watangazaji wasio na weledi, maadili, sifa na elimu ya Uandishi na Utangazaji wa Habari.

4.5 **Wasafi FM Radio** imeendelea kukiuka Sheria na Kanuni za Utangazaji licha ya juhudi za Kamati kukutana nao mara mbili; tarehe 11 Julai, 2023 katika ofisi za TCRA Makao Makuu na tarehe 25 Oktoba, 2023, Kamati ilipowatembelea katika ofisi zao Dar es Salaam, ambapo Kamati ilitoa elimu kwao kuhusu masuala ya msingi juu ya uandaaji na utoaji maudhui kwenye vyombo vya utangazaji.

## 5.0 USHAURI WA KAMATI KWA WASAFI FM RADIO.

5.1 Kamati inatambua kuwa suala la Utangazaji wa Habari linahitaji watu wenye sifa na elimu stahiki, maadili na weledi katika tasnia ya Uandishi na Utangazaji wa Habari. Hivyo, **Wasafi FM Radio** inashauriwa kuwa na watangazaji wenye sifa ili kukisaidia kituo hicho kisikiuke maadili, Sheria na Kanuni za Utangazaji.

5.2 Kutokana na kosa lililobainika, Kamati inaushauri Uongozi wa **Wasafi FM Radio** kuzingatia usimamizi na uhariri makini wa maudhui kabla ya kuyarusha ili kuhakikisha na kujiridhisha kuwa maudhui yao ni salama kisheria kabla ya kuyatangaza. Hatua hiyo itaiwezesha **Wasafi FM Radio** kuepuka kuvunja Sheria na Kanuni za Utangazaji.

5.3 Kamati inakishauri Kituo cha **Wasafi FM Radio** kuweka utaratibu wa ndani wa kuwajengea uwezo watendaji/watangazaji wake kwa kuwapatia mafunzo wakiwa kazini.

## 6.0 UAMUZI WA KAMATI

Baada ya kusikiliza na kutafakari kwa kina maelezo ya utetezi yaliyotolewa na Uongozi wa **Wasafi FM Radio**, na kwa kuwa Uongozi wa **Wasafi FM Radio** umekiri kukiuka Kanuni za Utangazaji katika kipindi husika, Kamati ya Maudhui imejiridhisha pasi na shaka lolote kuwa, pamoja na utetezi uliotolewa katika suala hili, **Wasafi FM Radio** imekiuka Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, 2018 kama zilivyofanyiwa marekebisho Mwaka 2020.

**Hivyo Basi**, kwa mujibu wa Kanuni ya 45 (3) (b) na (d) ya Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta kuhusu Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni, 2018 kama ilivyofanyiwa Marekebisho Mwaka 2020, Kamati ya Maudhui inaamua kama ifuatavyo:

1. **Wasafi FM Radio** kulipa faini ya **Shilingi Milioni Nne (TZS. 4,000,000.00)** tu, itakayolipwa kwa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) ndani ya siku thelathini (30) tangu kusomwa kwa uamuzi huu; na

2. **Wasafi FM Radio** inaamriwa kuomba radhi kwa wasikilizaji wao kwa muda wa siku tatu mfululizo kuanzia Jumatatu, tarehe 11 Desemba, 2023 mpaka Jumatano, tarehe 13 Desemba, 2023. Radhi hiyo itaombwa mwanzoni mwa kipindi chao cha ***Jana na Leo*** kilichotumika kutenda makosa hayo, kwa kusoma maneno yafuatayo:

    ***"Uongozi wa WASAFI FM RADIO unapenda kuomba radhi kwa wasikilizaji wetu wote ambao kwa namna moja au nyingine wamekwazika na maudhui yaliyotumia lugha isiyo sanifu, inayoweza kutafsiriwa kama matusi na yenye kuhamasisha ufanyaji wa ngono, hususan katika kipindi cha mvua, yaliyorushwa na Kituo chetu.***

***Maudhui ya kipindi hicho yalitangazwa tarehe 02 Novemba, 2023, katika kipindi chetu cha "Jana na Leo".***

***Tunafahamu kwamba kitendo hiki kimekiuka Sheria na Kanuni za Mawasiliano ya Kielektroniki na Posta (Maudhui ya Utangazaji wa Redio na Televisheni), 2018***

***Uongozi wa WASAFI FM RADIO unaahidi kuhakikisha kuwa Kituo kinafanya kazi kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Weledi kwa mujibu wa Maadili ya Uandishi wa habari na Utangazaji.***

***Tunaahidi kuwa kosa kama hili halitajirudia tena."***

Uamuzi huu umetolewa na kusomwa **Dar es Salaam,** leo tarehe **08 Desemba, 2023.**

Haki ya kukata rufaa dhidi ya uamuzi huu kwenye Baraza la Ushindani (Fair Competition Tribunal – FCT) iko wazi ndani ya siku ishirini na moja (21) kuanzia leo.

Uamuzi huu umesainiwa na:

MAMLAKA YA MAWASILIANO TANZANIA
20 BARABARA YA SAM NUJOMA
S. L. P. 474
14414 DAR ES SALAAM
TANZANIA

**Bi. Saida Mukhi**

..........................................................................

**Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maudhui, TCRA**

**PAMOJA NA WAJUMBE WA KAMATI YA MAUDHUI WAFUATAO:**

**Bw. Isaac Mruma** ..................................................

**Bw. Jacob Tesha** ..................................................